

EE YESU TUNAKULILIA.

Fabian Boma
Kilombero parish
03/03/2016

Kwa upole na utulivu

Ee Ye su Ee Ye su Ee Ye su Tu na ku li li a
Ye su wa_ ngu Ye su wa_ ngu Ye su

Ki fo cha ko ki na hu zu ni sha.

1.Ooh! Yesu wangu

Umekubali kuteswa kwa ajili ya dhambi zetu sisi wanadamu,
umekubali kupigwa, mpaka umekufa msalabani, ili uweze kutukombo. Ee Yesu utuhurumie.

2.Ooh! Yesu wangu

Kwa upendo ulionao kwetu sisi, ulitulisha mkate na samaki, ulimfufua Lazaro,
ulitunywesha divai kwenye harusi ya kana, ulitufundisha kusali umetufundisha tumjue Mungu Baba,
lakini leo tunakuua wenyewe. Ee Yesu utuhurumie.

3.Ooh! Yesu wangu

Umetuonesha ni jinsi gani unavyopetunda sisi wanadamu, na umetufundisha tupendane kama
Baba yetu wa mbinguni anavyotupenda, tunakuomba uendelee kutupenda. Ee Yesu utuhurumie.

4.Ooh! Yesu wangu

Petro alikukana yakuwa hakujui, nasisi Bwana tunakukana tunaposhindwa kukufuata,
Ooh! Yesu hii ni tafsiri yetu japo haijatokea kwenye vinywa vyetu, utujalie Ee Yesu ilitufe kifo chema.
Ee Yesu utuhurumie.

5.Ooh! Ee Yesu wangu

Kifo chako kinautikisa ulimwengu wote, ulimwengu mzima tunakulilia wewe Bwana,
kilio hiki sio cha jimbo letu pekee,
wala sio cha Tanzania pekee, na wala sio cha Afrika pekee bali ni kilio cha Dunia nzima,
tunakulilia wewe Bwana. Ee Yesu utuhurumie.